Toleo la 25

# jarida la WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Jarida la Mtandaoni | www.michezo.go.tz | Julai 01, 2022



# Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

# TAHARIRI

## UTAMADUNI CARNIVAL KIUNGO CHA UMOJA KWA WATANZANIA



Mhariri
**JOHN MAPEPELE**

Matembezi ya kiutamaduni yanayofanyika kesho Julai 2, 2022 jijini Dar es Salaam yaani Utamaduni carnival yamebeba sura ya umoja, uzalendo na mshikamano wa makabila yote ya Tanzania.

Matembezi hayo ya kihistoria yenye mvuto wa aina yake yatahusisha magari 31 yatakayokuwa na vikundi vya kiutamaduni kutoka mikoa yote nchini huku yakipambwa na burudani mujarabu inayotarajiwa kuwavuta wakazi wa jiji la Dar es salaam na viunga vyake vya manispaa za Temeke, Ilala, Ubungo, Kinondoni pamoja na Kigamboni.

Shamrashamra hizo zitaanzia Uwanja wa Uhuru kuelekea daraja la Mfugale, daraja la Kijazi Ubungo, Morocco, Namanga, Coco Beach, daraja jipya la Tanzanite, Posta, Kariakoo, Stesheni, Mtoni kwa Azizi Ally, Temeke, Mwembeyanga na kurudi Uwanja wa Uhuru.

Sisi Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, tunathamini Utamaduni wa taifa letu kwa kuzingatia kauli ya Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema "Utamaduni ni kiini ama roho ya taifa lolote, taifa lisilo na utamaduni ni sawa na mkusanyiko wa watu usio na roho."

Kila mmoja wetu anawajibu wa kulinda Utamaduni, kuendeleza na kuuhifadhi ndiyo maana tunasema "Utamaduni wetu; Fahari yetu; tujiandae kuhesabiwa, Kazi Iendelee".

**BODI YA WAHARIRI**

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
**Dkt. Hassan Abbasi**

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo
**Saidi Yakubu**

Mhariri
**John Mapepele**

Waandishi
**Eleuteri Mangi**
**Shamimu Nyaki**
**Eliphace Marwa**

Wapiga Picha
**Joseph Kigingi**
**Projestus Binamungu**

Msanifu
**Abubakar W Kafumba**



# Mhe. Mchengerwa kuteta na wanahabari kuhusu tamasha la Utamaduni leo

Na John Mapepele, **WUSM, Dar es Salaam**

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mhe. Mohamed Mchengerwa leo anatarajia kuwa na mkutano wa waandishi wa Habari ili kuzungumzia mageuzi na mapinduzi makubwa yanayofanywa na Serikali kwenye Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mkutano huo na wandishi wa habari unatarajiwa kufanyika majira ya saa 8:30 Alasiri Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam baada ya kukagua shughuli mbalimbali za Tamasha la Utamaduni la Kitaifa ambapo mikoa takribani yote ya Tanzania imeshafika.
Mhe. Mchengerwa amesema miongoni mwa shughuli zinazooneshwa kwenye uwanja huo kuwa ni pamoja na ngoma za asili kutoka makabila ya mikoa yote Tanzania na baadhi ya nchi za nje.

Ametoa wito kwa wananchi kuja kushuhudia tamasha hili la kihistoria ili kujifunza mambo mbalimbali ili kuendelea kuuenzi na kuutangaza utamaduni wa kitanzania kwa kuwa hakuna kiingilio, tamasha hilo ni bure hatua inayowapa watu wengi fursa ya kujifunza masuala mbalimbali ya kiutamaduni.

Kaulimbiu ya tamasha hili ni "Utamaduni wetu, Fahari yetu , Tujiandae kuhesabiwa, kazi iendelee!"



# Vikundi vya Utamaduni Vyawasili, Vyajipanga kukonga Nyoyo za Watanzania

Na Shamimu Nyaki - **WUSM, Dar es Salaam**

Vikundi vya Burudani vya makabila mbalimbali nchini vimewasili jijini Dar es Salaam tayari kwa ajili ya Tamasha kubwa la kihistoria la kwanza nchini linaloanza Kesho Julai 01, 2022.

Akizungumza na wana Utamaduni hao, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Saidi Yakubu amesema licha la vikundi hivyo kutoa burudani pia vitashiriki mashindano na washindi watapata zawadi na Vyeti kwenye kilele Cha Siku ya Kiswahili Julai 07, 2022.

"Naamini mmejiandaa kutoa burudani ya kutosha lakini pia mmejifua vyema Kwa ajili ya mashindano, na tayari majaji wamefika wapo tayari kutafuta mshindi. Naomba muitumie fursa hii vizuri ambayo sio tuu itawatangaza ndani ya nchi pia itakapotokea fursa nje ya nchi wizara itatafuta Kikundi ambacho kimeshinda kupitia mashindano haya kuliwakilisha taifa" amesema Naibu Katibu Mkuu Yakubu.

Ameongeza kuwa, Tamasha hilo litapambwa na Matembezi ya Kitamaduni yatakayozunguka jiji la Dar es Salaam na baadae kupokelewa Uwanja wa Uhuru na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa.
Tamasha hilo la siku tatu, litapambwa na Maonesho ya vyakula, ngoma na shughuli mbalimbali za Kitamaduni.




# Burundi watua Dar kushiriki tamasha la kitaifa la Utamaduni

Na John Mapepele, **WUSM, Dar es Salaam**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Maji na Madini nchini Burundi ndugu Selemani Khamissi ambaye pia ni mmiliki wa kikundi maarufu cha taarabu nchini humo cha Alwatan kinachoshiriki kwenye Tamasha la Kitaifa la Utamaduni ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuandaa tamasha hilo huku akisisitiza kuwa tamasha hilo litaitangaza vema Tanzania duniani.

Akiongea na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na michezo. Saidi Yakubu ofisini kwake jijini Dar es Salaam mara baada ya kuwasili amesema Serikali ya Burundi inaunga mkono jitihada za serikali ya Tanzania katika kuenzi na kuendeleza utamaduni ndiyo maana wasanii kutoka Burundi wanashiriki katika tamasha hili.

"Naomba nisema nimefurahi kuja Tanzania kushiriki kwenye tamasha tunawahidi watanzania wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kuja kuona uzoefu wetu kwenye taarabu kwa kuwa Burundi ina hazina kubwa ya magwiji wa taarabu kutoka miaka mingi" amesisitiza Khamisi.

Akiwa ofisini hapo Khamissi amepata fursa ya kutembelea Uwanja wa Benjamin Mkapa pia kuangalia maandalizi yanayoendelea ambapo ameelezea kuwa uwanja huo una hadhi ya kimataifa.

Akimtembeza kwenye miundombinu ya uwanja huu Yakubu amesema maandalizi kwa ajili ya tamasha hilo yamekamilika.



# Maandalizi ya Tamasha la Utamaduni Kitaifa Yapamba Moto

Na Eliphace Marwa – **WUSM, Dar es Salaam**

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imeendelea na maandalizi ya Tamasha la Utamaduni Kitaifa linalotarajiwa kufanyika kuanzia kesho Julai Mosi mpaka Julai Tatu katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Wasanii kutoka sehemu mbalimbali za nchi wamewasili jijini Dar es salaam tayari kwa tamasha hilo la kihistoria hapa nchini Tanzania.

Akizungumza mara baada ya kuwasili katika Uwanja wa Uhuru, Mwenyekiti wa Mila na Desturi toka Mkoa wa Morogoro, Chifu Ramadhan Divunyagale amesema kuwa Serikali ya awamu ya sita chini ya ungozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kupitia Wizara ya Utamaduni, Saanaa na Michezo imefanya kazi kubwa ya kuwakutanisha.

"Tunaishukuru Serikali kwa kuweza kutukutanisha pamoja kwani tutapata nafasi ya kubadilishana na kupeana uzoefu wa mila tofautitofauti na kuweza kuwarithisha vizazi vijavyo," alisema Mwenyekiti huyo.

Kwa upande wake mmoja wa washiriki toka mkoani Mbeya, Ambakisye Mwamwaja amepongeza Wizara kwa kuweza kufanikisha tamasha hili la Utamaduni wa Kitaifa.

"Kwa kweli maandalizi ni mazuri naamini ushindani utakuwa ni mkubwa kwani naona kila mkoa umejipanga kushinda katika tamasha hili la Utamaduni wa Kitaifa," alisema Bw. Ambakisye.

Tamasha hilo litajumuisha wasanii na Machifu wa mikoa yote ya Tanzania ambapo kutakuwa na maonesho ya ngoma za makabila mbalimbali, mapishi ya vyakula vya asili toka mikoa yote itakayo shiriki tamasha hilo pamoja na burudani mbalimbali ikiwemo usiku wa Taarab utakao fanyika siku ya Julai 3 katika ufukwe wa Coco Beach jijini Dar es Salaam.

Katika Tamasha hilo linatarajiwa kufunguliwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mb) siku ya Julai 2 na kufungwa na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mussa Azan Zungu Siku ya Julai tatu jijini Dar es Salaam.





# Safari Kubwa ya Mageuzi ya Kuimarisha Utamaduni Yapamba Moto Nchini

Na Eleutri Mangi - **WUSM, Dar es Salaam**

Chifu Jabiri Shaban Msofe kutoka Mwanga mkoani Kilimanhjaro amesema Tamasha la Utamaduni la Kwanza Kitaifa linaleta mwamko mpya wa kiutamaduni ambao unajenga umoja kwa kuwaleta Watanzania pamoja kwa wakai mmoja.

Chifu Msofe amesema hayo Juni 30, 2022 akiwa wilayani Mwanga alipofanya mahojiano kwa njia ya simu na mwandishi wetu akiwa jijini Dar es Salaam ambapo amesema safari kubwa ya mageuzi ya kuimarisha utamaduni inayofanywa na serikali imepamba moto nchini na kuwa darasa kwa vijana wanaokua.

"Huu mwaliko wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo tumeupokea kwa mikono miwili, tunakutana wote nchi nzima, tupo wamoja. Wasiojua utamaduni wao watajifunza huu ni ukurasa mpya kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo" amesema Chifu Msofe.

Chifu Msofe ameongeza kuwa Serikali ya Awamu wa Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muiungano wa Tanzania kwa kuendelea kuthamini, kulinda na kuendeleza utamaduni wa mtanzania wakati wote.

Aidha, Chifu Msofe amesisitiza kuwa, huo ni mwanzo mzuri wa safari kubwa ya kuimarisha utamaduni kwa kuwa matamasha hayo yatainua na kuibua hazina kubwa ya kiutamaduni miongoni mwa jamii nchi nzima na yana tija kwa kuleta taifa.


WIZARA YA UTAMADUNI
SANAA NA MICHEZO
KUELEKEA SIKU YA KISWAHILI DUNIANI
JULAI 7, 2022 JNICC DAR ES SALAAM
UZINDUZI WA TAMASHA LA KWANZA KITAIFA LA UTAMADUNI
MGENI RASMI
Mhe. KASSIM MAJALIWA
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Julai 2, 2022
MUDA: Saa 8:00 Mchana
MAHALI: Uwanja wa Uhuru Dar es salaam
KAULI MBIU: Utamaduni Wetu; Fahari Yetu; Tujiandae Kuhesabiwa, Kazi Iendelee".
Wizara-Sanaatz
SanaaTv


WIZARA YA UTAMADUNI
SANAA NA MICHEZO
KUELEKEA SIKU YA KISWAHILI DUNIANI
JULAI 7, 2022 JNICC DAR ES SALAAM
NITAKUWEPO
KONGAMANO LA MCHANGO WA KISWAHILI KWENYE UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA
MUSSA AZZAN ZUNGU
Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Julai 6, 2022
JNICC DAR ES SALAAM
KAULI MBIU: Utamaduni Wetu; Fahari Yetu; Tujiandae Kuhesabiwa, Kazi Iendelee".
Wizara-Sanaatz
SanaaTv


WIZARA YA UTAMADUNI
SANAA NA MICHEZO
KUELEKEA SIKU YA KISWAHILI DUNIANI
JULAI 7, 2022 JNICC DAR ES SALAAM
NITAKUWEPO
KONGAMANO LA MCHANGO WA KISWAHILI KWENYE UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA
ABDULRAHMAN KINANA
Makamu Mwenyekiti wa CCM-Bara
Julai 6, 2022
JNICC DAR ES SALAAM
KAULI MBIU: Utamaduni Wetu; Fahari Yetu; Tujiandae Kuhesabiwa, Kazi Iendelee".
Wizara-Sanaatz
SanaaTv


WIZARA YA UTAMADUNI
SANAA NA MICHEZO
KUELEKEA SIKU YA KISWAHILI DUNIANI
JULAI 7, 2022 JNICC DAR ES SALAAM
NITAKUWEPO
KONGAMANO LA MCHANGO WA KISWAHILI KWENYE UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA
AME MPUNGWE
Balozi Mstaafu
Julai 6, 2022
JNICC DAR ES SALAAM
KAULI MBIU: Utamaduni Wetu; Fahari Yetu; Tujiandae Kuhesabiwa, Kazi Iendelee".
Wizara-Sanaatz
SanaaTv


WIZARA YA UTAMADUNI
SANAA NA MICHEZO
KUELEKEA SIKU YA KISWAHILI DUNIANI
JULAI 7, 2022 JNICC DAR ES SALAAM
NITAKUWEPO
KONGAMANO LA MCHANGO WA KISWAHILI KWENYE UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA
Mhe. NAPE MOSES NNAUYE (Mb)
Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari
Julai 6, 2022
JNICC DAR ES SALAAM
KAULI MBIU: Utamaduni Wetu; Fahari Yetu; Tujiandae Kuhesabiwa, Kazi Iendelee".
Wizara-Sanaatz
SanaaTv


WIZARA YA UTAMADUNI
SANAA NA MICHEZO
KUELEKEA SIKU YA KISWAHILI DUNIANI
JULAI 7, 2022 JNICC DAR ES SALAAM
NITAKUWEPO
KONGAMANO LA MCHANGO WA KISWAHILI KWENYE UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA
ZITTO KABWE
Kiongozi wa ACT WAZALENDO
Julai 6, 2022
JNICC DAR ES SALAAM
KAULI MBIU: Utamaduni Wetu; Fahari Yetu; Tujiandae Kuhesabiwa, Kazi Iendelee".
Wizara-Sanaatz
SanaaTv

# WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano
Serikalini - GCU

**Mawasiliano**
P.O. Box 25, Dodoma,Tanzania
Mji wa Serikali Mtumba
Telephone: +255 26 2322 129
Nukushi: +255 26 2322 128
Barua pepe: km@habari.go.tz